


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anatangaza nafasi za kazi kwa wakazi wa Wilaya ya Kyela wenye uwezo na uzoefu wa kazi ya kukusanya ushuru (Revenue Collectors) katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama ifuatavyo:-

1. MTOZA USHURU WA HALMASHAURI (REVENUE COLLECTOR)
IDADI YA NAFASI: 50

Sifa za mwombaji

- i. Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- ii. Awe Raia wa Tanzania
- iii. Awe mkazi wa Wilaya ya Kyela
- iv. Awe na umri kuanzia miaka 18-45
- v. Mwombaji awe na wadhamini wawili (2) kila mdhamini anatakiwa kuwa na hati ya mali isiyohamishika
- vi. Barua za maombi zote zipitishwe kwa Mtendaji wa Kijiji au Mwenyekiti wa Kijiji anapoishi na Mtendaji wa Kata husika.
- vii. Picha mbili za (Passport size) rangi yoyote
- viii. Mdhamini ambaye siyo Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ataambatanisha barua ya utambulisho toka kwa mwajiri wake.
- ix. Mwombaji ataandika juu ya bahasha majina kamili na Kata anayotoka.

2. MUHIMU

Tangazo hili linawahusu pamoja na Watumishi/Watoza ushuru wote wanaendelea na kazi ya kutoza ushuru kwa **sasa katika vyanzo mbalimbali vya Halmashauri.** (Wote wanapaswa kuomba upya)

3. MASHARTI YA KAZI

Kazi hii itakuwa ni ya Mkataba wa **miezi sita (6)** na mkataba unaweza ingiwa upya) au kutangaza nafasi husika upya kulingana na mahitaji ya Halmashauri ya Kyela.

Malipo kwa mtoza ushuru yatalipwa kulingana na makusanyo kwa asilimia kumi (10%) ya makusanyo ya chanzo husika.

Maombi yote yawasilishwe kwa anuani husika.

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Kyela
S.L.P. 320,
KYELA.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 23.01.2025 saa tisa na usu (9:30) Alasiri.

Imetolewa na:

Florah .A. Luhala
MKURUGENZI MTENDAJI(W)
KYELA

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYI
KYELA**